**BUKOBA HOPE LUTHERAN SECONDARY SCHOOL (BUHOLUSE)**
ELCT - NORTH WESTERN DIOCESE
P.O. Box 1425, Bukoba, Tanzania; **Phone**: +255 754 264 200/+255 28 222 0027
**Email**: bhl.nwdelct@gmail.com **Website**: www.bukobahopelctnwd.ac.tz
**Physical Address**: *Bukoba Town-Biharamulo-Kyetema-Kanazi-Ibwera-Ruhija Road:* **38 Kms**
**Motto: Where Everyone is in Christ, Everyone Wins**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2024

**{Ambaye hakufanya mtihani wa kujiunga atalipa sh. 10,000/= kwa ajili ya usajili shuleni}**

Mpendwa mwanetu: **…………………………………………………………………………………………….**

## 1.0 UTANGULIZI

Tunafurahi kukujulisha kuwa unazo sifa na umechaguliwa kujiunga Kidato cha I mwaka **2024** katika Shule ya Sekondari **Bukoba Hope Lutheran**. Shule inapokea mtoto wa dini na kabila lolote. Hongera sana maana Mungu amekujalia kuwa miongoni mwa wanafunzi katika shule hii inayoongozwa Kikristo kwa ajili ya malezi na taaluma bora. Jina letu maarufu ni **Familia ya Washindi** maana hapa mtoto hushinda Kitabia na Kitaaluma. Ni familia ambayo wanetu huitana Kaka na Dada bila kujali umri. Bila shaka umesikia maisha haya ukaamua kuichagua familia yetu. Basi, ninakuomba uripoti shuleni tarehe **04/01/2024 Alhamisi**. Muda wa kufika ni tangu saa 1.30 asubuhi kila siku hata siku za mapumziko. Masomo yataanza **05/01/2024** kwa kuwa huwa hatusubiri waliochelewa. Ibada ya ufunguzi na itakuwa tarehe **07/01/2024**. Tutaalika Kwaya na Mhubiri kwa siku hiyo maalum.

Ninaomba wazazi wasome vizuri maelekezo haya. Jambo mojawapo zuri watakalogundua ni kuwa karo ya shule yetu ni ndogo. Kwanini? Karo yetu imeunganishwa na michango mingine na inalipwa pole pole. Kwetu, fedha utakazosoma baadaye nje ya jedwali la karo, kimsingi zinatumiwa moja kwa moja na mwanafunzi, si za shule. Mfano sare, Biblia, vyombo vya chakula, na Bima.

Tunafundisha masomo tisa ya kawaida kwa kila shule. Tunaongeza somo la Bible Knowledge na Computer. Shule yetu si ya ufundi au VETA ila kutokana na kilio cha taifa cha watoto kuhitimu bila ujuzi wowote, tumeanzisha masomo ya ujuzi mdogo mdogo kwa muda wa ziada. Utachagua mwenyewe ujuzi unaopenda. Ukiupata mmoja, unaweza kuchagua ujuzi mwingine. Masomo ya Ujuzi ni *Useremala, Muziki, Kufuma, Michezo, Kushona, Ujenzi, Fundi Bomba, Mazingira, Umeme, Kupamba, na Mapishi.* Aidha, ufahamu kuwa shule nyingi wanafunzi wakifika Kidato cha III huamua kutosoma masomo ya Sayansi. Unayo bahati kwa kuwa kwetu masomo ya Sayansi ni lazima tangu Kidato cha I hadi cha IV. Lengo letu ni kuhakikisha wanetu wanafungua milango yote miwili, yaani Sayansi na Sanaa. Tuseme, kwetu Sayansi na Hisabati "ndiyo habari ya mjini". Ukifika Januari, 2024, utaona ukweli huo.

### 1. 1 Mahali na Usafiri

Bukoba Hope Lutheran ipo umbali wa Kilometa 38 kutoka Manispaa ya Bukoba kwenye Halmashauri ya Bukoba. Ukitokea kituo cha mabasi Bukoba utapanda Hiace ziendazo uelekeo wa Izimbya, Kikomero, au Katoro. Nauli ni Sh. **3,000/=** Utashuka Ibwera na kupanda pikipiki kwa **sh. 1,500/= au 2,000/=.** Kilometa 3 kutoka Ibwera, tayari utajikuta umefika kilimani penye miti na upepo safi, kwenye "Bustani ya Edeni" yaani Bukoba Hope. Utapokelewa kwa tabasamu la wanafamilia wenye upendo mwingi kwako kwa kukubali kujiunga na Familia yao ya Washindi.

Gharama za safari kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo zinalipwa na mzazi au mlezi wa mwanafunzi. Hata hivyo, wakati wa kwenda na kutoka likizoni, wanetu husafiri kwa pamoja. Wanaopitia Bukoba Mjini hufikishwa kwenye magari ya kwao, na wakati wa kurudi wanetu hupokelewa TTCL Bukoba Mjini. Basi, TTCL ndiyo kituo cha familia yetu tunaposafiri likizoni. Wazazi wa mbali hawafuati na hawaleti watoto shuleni likizoni kwa kuwa pia tunapanga vizuri utaratibu wa usafiri. Tuko tayari kufanya mpango wa usafiri kwa mtoto tunayejulishwa kuwa atafika muda ambao magari ya abiria yameishafunga huduma hiyo.

## 2.0 MAHITAJI MUHIMU

**2.1 Karo na Michango** ***Haijawahi kubadilika tangu mwaka 2017!

| KIPENGELE | MUHULA I | | MUHULA II | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| | Januari - Machi | Aprili - Juni | Julai - Agosti | Sept. - Novemba | |
| Karo | 410,000/= | 225,000/= | 400,000/= | 225,000/= | |
| **Jumla** | **410,000/=** | **225,000/=** | **400,000/=** | **225,000/=** | **1,260,000/=** |

***Michango ambayo hatupangi sisi kama vile ya mitihani ya nje na ya michezo, tutawajulisha wazazi ukishajiunga, na tukiwa tumeishajulishwa rasmi na wahusika.**

Malipo yote yaliyoandikwa katika maelekezo haya ambayo hatukuandika kuwa unaweza kuleta shuleni, yafanyike kupitia benki **CRDB Bukoba, Tawi lolote la CRDB, au FAHARI HUDUMA (***mwenye mashine inayoandika jina la mwanafunzi***). Jina la akaunti ni BUKOBA HOPE LUTHERAN SEC. A/C. Na. 0150285841800.** Leta hati ya malipo “Pay-in-slip” ikiwa na jina la mwanafunzi na kidato chake vilivyoandikwa na benki kwa mashine.

**Muhimu sana**: (i) Kuna shule nyingi zinaitwa ‘Bukoba’. Hii uliyochaguliwa ni Bukoba **Hope**.
(ii) Mtoto akiacha masomo hapa shuleni kwa sababu zake binafsi hatarudishiwa fedha kutoka shuleni.

**2.2 Mahitaji Mengine**

- Kadi ya Bima ya afya ya taifa ya **NHIF** au kama huna **leta sh. 50,400/= ili tukutafutie Bima hii.** Fedha hizi zitalipwa kila mwaka. Ni fedha za serikali wala shule haibaki na senti hata moja. Bima ni lazima kwa kila mtoto ili tuwe na uhakika wa afya ya mtoto. Wazazi wengine husita kuilipa ila mtoto anapougua wakatumia hela nyingi hujuta. Basi hatutaki majuto haya maana ugonjwa haubishi hodi.
- Fedha ya Kitambulisho **sh. 5,000/=**
- *Glory to God* (kitabu kidogo cha ibada cha Kiingereza) – utauziwa shuleni kwa **Sh. 3,000/=.**
- Vyombo vya chakula vyote ili vifanane tena vya kula kisasa. **Fedha ziletwe shuleni Sh. 8,000/=.**
- Rimu mbili za karatasi A4 zisizo na mistari. Waweza kuleta moja Januari, nyingine Julai.
- **Matokeo yako ya Darasa la Saba**. Ukiyapata shuleni yathibitishwe na Mwl. Mkuu au Kiongozi mwingine wa Elimu. Ukiyapata mtandaoni hayahitaji kuthibitishwa. Usipoyaleta utalipa hela.
- Fyekeo moja (usilete kotama).
- Mpini mmoja wa jembe (usilete jembe maana tunayo mengi).
- Mfagio wa nje wenye mpini (chelewa yenye mpini).
- Nakala ya cheti cha kuzaliwa maana kuna wanafunzi wanachanganya tarehe zao za kuzaliwa.

**2. 3 Mahitaji Binafsi**

- ✓Biblia ya Kiingereza iitwayo RSV ni lazima mno **(ikiwa hautaifahamu Biblia ya RSV leta shuleni hela isiyozidi sh. 18,000/= tutasaidia kuinunua). Ukiamua kuleta hela hii ya Biblia, usiiweke benki.**
- ✓Truck-suit leta shuleni **sh. 25,000/=** tutanunua kwa pamoja ili iwe sare na tuepuke mchanganyiko wa rangi.
- ✓Fedha ya kuweka alama kwenye nguo zako **sh. 6,000/=**
- ✓Ukiamua kutoleta matokeo ya darasa la saba, itabidi ulipe **sh. 1,000/=** ukifika
- ✓Mchango wa Mahafali ya Dini na Shule Kidato IV utapangwa ukiwa shuleni ; utajulishwa ukishafika.
- ✓Kamusi kubwa ya Kiingereza tu (hasa inayoanzia bei ya sh. 25,000/= ila uinunue usilete hela shuleni)
- ✓Mfuko wa kubebea madaftari
- ✓Nguo za ndani na nguo za kuvaa ili kulala.

  **Muhimu**: (i) Msichana **lazima** awe na nguo nyepesi nyeupe au nyeusi (isiwe t-shirt) isiyo na maandishi wala picha ya kuvaa ndani ya shati.
  (ii) Mvulana ikiwa atapenda kuleta nguo ya kuvaa ndani ya shati, basi iwe nguo nyepesi nyeupe au nyeusi (isiwe t-shirt) isiyo na maandishi wala picha.
- ✓Kandambili
- ✓Taulo (Ila msichana anaruhusiwa pia kuleta kitenge kimoja au khanga moja)
- ✓Sabuni za kutosha
- ✓Mafuta ya kujipaka
- ✓‘Toilet paper’ za kutosha (utazitunza mwenyewe)
- ✓Sanduku imara lenye kufuli (wengi huleta ya bati)
- ✓‘Box file’ moja kwa ajili ya kutunzia kazi zako (utalitunza wewe)
- ✓Mkebe wa Hesabu, rula ya inchi 12, kalamu za wino wa bluu au mweusi, na kalamu za risasi
- ✓Madaftari makubwa (counter book Q. 2 au zaidi) 12 na madaftari mengine madogo ya kutumia unapojisomea binafsi.
- ✓Daftari ziitwazo ‘Graph pads’ 2 au zaidi (utazitunza mwenyewe kwa kazi binafsi za kitaaluma).

**KARO YETU NI NAFUU ZAIDI YA WENGINE KWA SABABU ZIFUATAZO**

- **Utapata dawa za msingi shuleni bila kulipia. Maana yake gharama hizi ziko kwenye karo.**
- **Ukiugua tukakupeleka kutibiwa vituo jirani au hospitali za hapa Bukoba, shule italipa nauli yako na nauli ya mfanyakazi atakayekusindikiza maana sisi mtoto lazima asindikizwe. Ukilazwa, mfanyakazi au mwanafunzi atabaki kukuhudumia hadi tutakapowapata wazazi. Kawaida hatuiti mzazi kabla sisi hatujampeleka mtoto hospitalini. Hii ni kwa kuwa sisi ndiyo Familia ya mtoto akiwa shuleni.**
- **Hatuombi litokee lakini ukifiwa na mzazi, mlezi, kaka, au dada, ukiwa wa karibu tutakusindikiza. Ukiwa wa mbali, mfanyakazi mmoja au wawili watakusindikiza, shule italipa nauli yote ikiwemo hata ya kurudi kwako na matumizi ya njiani. Haya ndiyo maisha ya Kifamilia.**
- **Baba au Mama akifiwa na Mzazi wake (Babu au Bibi yako), shule itatoa rambirambi ya sh. 50,000/=**
- **Ndoo utaazima shuleni ikiwa ni shukrani kwa kuichagua Familia ya Washindi.**
- **Jembe utaazima shuleni ikiwa ni shukrani kwa kuichagua Familia ya Washindi.**
- **Chandarua utaazima shuleni ikiwa ni shukrani kwa kuichagua Familia ya Washindi.**
- **Godoro utaazima shuleni bila malipo ikiwa ni shukrani kwa kuichagua Familia ya Washindi.** Ila mtoto anayekojoa kitandani ni lazima alete godoro lake imara lisilo chakavu. Godoro ni futi 2.5 kwa futi 6.
- **Utatumia majengo na viti na meza bila kuchangia maana yote haya yako kwenye karo yetu.**
- **Utasoma Sayansi na 'Computer' kwa vitendo bila malipo ya ziada. Utalipia Sayansi ukiwa Kidato cha IV.**
- **Mzazi anaweza kuomba kuwa na awamu zake za kulipa ada kadri ya uwezo wake ilimradi amalize ada yote tarehe 15/11/2024. Hata hivyo, ili kuhakikisha shughuli za shule hazikwami, mzazi akitaka utaratibu huu, ataleta barua kwa Mkuu wa Shule siku ya kukuleta mtoto ili kushauriana na kukubaliana kuhusu awamu alizoweka. Njia hii imesaidia wazazi wenye uwezo mdogo kulipa ada bila shida hasa wale ambao uheshimu na kufuata awamu hizo kwa kupunguza fedha kidogo kidogo.**

## 2.4 Sare ya Shule

### 2.4.1 Sare muda wa ibada, darasani, mikutano rasmi, na nje ya shule

| MSICHANA | MVULANA |
|---|---|
| Mashati 3: leta shuleni sh. **34,000/=.** | Mashati 3: leta shuleni sh. **34,000/=.** |
| Sketi 2: leta shuleni sh. **31,000/=.** | Suruali 2: leta shuleni sh. **35,000/=.** |
| Soksi nyeupe zisizo na matundu jozi 3 | Soksi nyeupe zisizo na matundu jozi 3 |
| Viatu vyeusi vilivyofunikwa vyenye visigino vifupi (sentimeta 2) – visiwe simple au bajaji | Viatu vyeusi vilivyofunikwa vyenye visigino vifupi (sentimeta 2) – si mchongoko. |
| Sweta 1: leta shuleni sh. **20,000/=** | Sweta 1: leta shuleni sh. **20,000/=** |
| Tai 1: leta shuleni sh. **4,000/=** | Tai 1: leta shuleni sh. **4,000/=** |
| T-shirt rasmi ya shule: leta sh. **15,000/=** | T-shirt rasmi ya shule: leta sh. **15,000/=** |

***Shati moja litakuwa la mikono mirefu kwa ajili ya ibada na ziara za nje ya shule.**

### 2.4.2 Sare nje ya muda wa vipindi na wakati wa kazi za nje

| MSICHANA | MVULANA |
|---|---|
| Sketi 1 dark blue – solo inayofunika magoti. Shona na uje umeivaa siku ya kuripoti. | Suruali 1 dark blue isiyobana. Shona na uje umeivaa siku ya kuripoti. |
| T-Shirt 2: nunua rangi ya njano zisizo na maandishi yoyote wala kola. (*Vaa moja wakati wa kuripoti shuleni).* | T-Shirt 2: nunua rangi ya kijani zisizo na maandishi yoyote wala kola. (*Vaa moja wakati wa kuripoti shuleni).* |
| Bukuta nyekundu kwa ajili ya michezo (isiyombana sana) | Bukuta ya bluu kwa ajili ya michezo. |
| Raba kwa ajili ya michezo. | Raba kwa ajili ya michezo. |
| Jozi moja ya viatu rahisi 'Simple open shoes' | Jozi moja ya 'Simple open shoes' |

*** Bukta na t-shirt anaweza kuleta idadi zaidi ya tulizotaja. Sisi tumelenga uwezo wa wazazi wengi.**

**2. 5 Malazi**

- Mto, foronya 2 (moja bluu bahari na nyingine pinki), blanketi 1, na mashuka 2 (moja pinki na jingine bluu bahari). **Muhimu**: Shuka liwe refu kiasi cha kukunjiwa chini ya godoro kichwani na miguuni. *Huu ni urefu usiyo chini ya mita 2 na robo.*

**2.6 Vifaa Utakavyoazima Shuleni**

Kila kifaa utakachoazima au kukabidhiwa shuleni itakubidi ukitunze vizuri. Kikiharibika au ukikipoteza utalazimika kukilipia. Kwa kawaida ukiharibu au kupoteza kitu kimoja, utalipa viwili isipokuwa kitabu utalipia tu idadi uliyoharibu au kupoteza.

*****Ukipata maelekezo haya kwa njia ya mtandao au njia nyingine nje ya shule na ulikuwa hujalipa sh. 10,000/= za maombi ya nafasi, basi utazilipa ukiripoti shuleni. Maelekezo haya yenye sahihi ya Mkuu wa Shule ni kwa ajili tu ya wanafunzi ambao tayari wamechaguliwa na kuandikwa kwenye orodha ya waliofaulu shuleni. Hawa wametumiwa kwa njia ya mtandao/simu.**

Rev. J. Mwesigwa Kyaruzi
**MKUU WA SHULE 0754 264 200 / 0759742310**

## SHERIA ZA SHULE

**1. NIDHAMU, MAADILI, NA IBADA**

**Bukoba Hope Lutheran** ni shule yako. Asante kwa kuchagua 'kijito cha malezi' ambapo ukweli, kuabudu, uaminifu, upendo, amani, na uwajibikaji ni tunu zake. Kwa hiyo, pamoja na kwamba umetumiwa sheria za shule, ni muhimu kuzingatia tunu hizi moyoni mwako na kuzifuata bila shuruti maana ndizo msingi wa sheria ulizopewa. Lengo la Bukoba Hope ni kuunda tabia njema zitokazo moyoni. Unapaswa kuhudhuria ibada siku ya Bwana na nyinginezo. Aidha unapaswa kuhudhuria sala za pamoja za asubuhi na jioni kila siku bila kusubiri kulazimishwa. Kupitia sala na ibada za pamoja, tunalenga kujenga umoja wa watanzania katikati ya imani yao kwa Mungu. Ili kujenga nidhamu na maadili, **hapa Bukoba Hope, familia nzima inatambua kuwa 'maisha ni ibada'.**

**2. USAFI**

Unatakiwa kuwa nadhifu wakati wote. Nguo za heshima, usafi wa mwili na roho, na kutunza mazingira ni mambo ambayo tutazingatia mno ili ukirudi nyumbani familia yako na jamii wakuone kwamba hukutoka kwenye chemichemi ya taaluma tu bali pia ya malezi. Ukipita sehemu ukatupa takataka au ukaacha takataka, utakuwa unawahuzunisha wote waishio hapa tunakotaka pawe kweli **'Bustani ya Edeni'.**

**3. TAALUMA NA LUGHA RASMI**

Umeamua kujiunga na Bukoba Hope kwa lengo kuu moja, yaani kujifunza. Utahitajika kutimiza yote yahusuyo taaluma bila kutegea. Sharti ufanye jitihada katika taaluma, uhudhurie vipindi, uwahi darasani, uwe makini mwalimu anapofundisha, uulize maswali usipoelewa, usitoroke, ufanye mazoezi na majaribio yote unayopewa. Huruhusiwi kupiga kelele au kuwasumbua wenzio darasani. Alama za ushindi kwa kila somo ni 55%. Ukipata alama za chini itakubidi ama urudie mtihani, urudie darasa, au uhamie shule nyingine. Hata hivyo, hatutegemei mwanafunzi ashindwe mitihani kwa kuwa tumedhamiria kuwasaidia sana wenye uwezo mdogo kitaaluma.

Unapaswa kutumia lugha ya Kiingereza wakati wote ukiwa hapa shuleni kwa sababu tunakuandaa uwe msomi wa Kimataifa. Licha ya kuwa lugha rasmi ya mawasiliano, Kiingereza ni lugha inayotumika kufundishia masomo yote isipokuwa somo la Kiswahili. Hivyo, lugha ya Kiingereza inatiliwa mkazo sana. Usipoiongea kwa hiari, tutakulazimisha. Mkakati wa Kiingereza utawashangaza mno waliosoma shule zisizotumia Kiingereza kwa kuwa kwa mwaka mmoja, tayari watakuwa wanaongea Kiingereza kama waliosoma 'English Medium'.

## 4. MKATE WA KILA SIKU

Kabla hujaanza safari kuja shuleni, tafuta Biblia ya Kiingereza, kaa na familia yako, chagua mstari mmoja mfupi, uandike ulivyo kwa Kiingereza. Ukifika shuleni utaukariri ili uwe mwongozo wako katika maisha yako shuleni na nje ya shule. Kwa hiyo chagua mstari unaozungumza nawe na kukuelekeza vema. Kila nusu muhula tunakuwa na mstari wa Biblia wa kuiongoza familia yetu. Basi, mkate wetu wa kila siku ni Neno la Mungu.

**Tunakutakia maandalizi mema na safari njema. Karibu sana kwenu tujenge Familia moja ya Washindi. Tunakusubiri kwa shauku kwa sababu tunakupenda (We love you).**

## 5. UVAAJI NA VIPODOZI SHULENI

i) Wakati wa masomo au unaporuhusiwa kutoka nje ya shule unapaswa kuvaa sare ya shule.
ii) Baada ya masomo unapaswa kuvaa sare ya shughuli za nje ya darasa au sare ya michezo wakati wa michezo. Hakuna nguo nyingine ya nyumbani inavaliwa shuleni labda kwa kibali maalum sana.
iii) Wakati wa mahafali utapaswa kuvaa sare ya shule.
iv) Huruhusiwi kutumia vipodozi na marashi ukiwa shuleni.

## 6. KUTEMBELEWA NA WAGENI SHULENI

Utaruhusiwa kutembelewa na wazazi/walezi au jamaa walioorodheshwa kwenye fomu iliyoambatishwa hapa kwa tarehe itakayotangazwa. Utaruhusiwa kuongea na wageni wako kwenye sehemu iliyoandaliwa kwa mapokezi tu. Wageni wako wavae kiheshima wanapokuja shuleni. Siku ya kukutembelea, hawataleta vyakula vilivyopikwa kama wali na ndizi bali vyakula vikavu na vinywaji baridi. Hata hivyo, siku hiyo wakileta zawadi hiyo, wanatakiwa kutenga pia zawadi kwa ajili ya familia nzima, kwa maana si watoto wote hutembelewa. Tofauti yetu na shule nyingine, Bukoba Hope tusemapo tunaishi kifamilia, tunataka hata wazazi wawafikirie watoto wengine katika familia yetu.

## 7. KWENDA NJE YA SHULE

Ukiwa na shida ya kukulazimisha kwenda nje ya shule sharti uombe ruhusa na kupewa kibali maalum. Ni kosa kwenda nje ya shule bila ruhusa na karatasi ya kibali.

## 8. MISEMO AU KAULI ZA MALEZI SHULENI

Tunasema tumia hekima na busara katika maamuzi nyeti hata kama kuna sheria au hakuna sheria kuhusu jambo hilo. Aidha, ukifika katika familia yetu utakutana na misemo au kauli hizi za kimalezi**: SHULE POLE POLE** – Maana yake ukiwa mgeni, tulia ili ujifunze tunavyoishi. **Ma Badi**: Ufupi wa jina la mwanamke mmoja Marehemu Baldiana Ngeiyamu aliyewalea wanae akiwambia kuwa kuna mambo mawili ya lazima katika maisha lakini hayafundishwi shuleni, kwa Kiingereza ni *Common sense* na *Sense of responsibility* (Kiswahili huenda ni Akili ya kuzaliwa na Moyo wa kujituma). Msemo mwingine ni **SISI NI FAMILIA YA WASHINDI** ukilenga ushindi wa tabia na kitaaluma. Mwisho ni Neno la Mungu kwenye mazingira yetu lisemalo, **FOR GOD'S TEMPLE IS HOLY, AND THAT TEMPLE YOU ARE**. Lengo ni kumtaka kila mwanafamilia kulinda mwili wake usichafuke kiroho. Misemo hii ni muhimu sana kuliko sheria katika kujenga familia yetu.

## 9. MAKOSA YANAYOWEZA KUMFANYA MWANAFUNZI AFUKUZWE SHULE

a) Kukiuka sheria za shule.
b) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule au ya wenzake.
c) Kuwagomea viongozi.
d) Kuwatukana au kuwapiga wenzake na watu wengine.
e) Ulevi, uvutaji wa sigara, bangi au utumiaji wa madawa ya kulevya
f) Uasherati
g) Wizi
h) Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa Shule au Makamu Mkuu wa Shule.

i) Utoro wa aina yoyote kama vile kutokuwemo darasani unapotakiwa kuwa darasani, kutoka nje ya shule bila kibali, na kwenda sehemu tofauti na uliyoruhusiwa kwenda.
j) Kuwa na simu, redio au kamera shuleni. Mawasiliano yote yatapitia kwa Mkuu wa Shule au atakayepewa jukumu hilo na Mkuu wa Shule.
k) Udanganyifu kwenye mitihani na majaribio. Adhabu yake ya haraka ni kurudishwa nyumbani kwanza kwa siku zisizopungua 21.
l) Kushindwa kutumia hekima na busara katika maamuzi nyeti.

*****Ukipata maelekezo haya kwa njia ya mtandao au njia nyingine nje ya shule na ulikuwa hujalipa sh. 10,000/= za maombi ya nafasi, basi utazilipa ukiripoti shuleni. Maelekezo haya yenye sahihi ya Mkuu wa Shule ni kwa ajili tu ya wanafunzi ambao tayari wamechaguliwa na kuandikwa kwenye orodha ya waliofaulu shuleni. Hawa wametumiwa kwa njia ya mtandao/simu.**

Rev. J. Mwesigwa Kyaruzi
**MKUU WA SHULE** **0754 264 200 / 0759742310**

## TAARIFA MAALUM KUHUSU MWANAFUNZI

### 1. HISTORIA YA MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi ……………………………………........................................................................................
Tarehe ya kuzaliwa ……………………………….................................................................................................
Kijiji/Mtaa……………………........................Wilaya……….........……………......Mkoa …............…………....

Shule aliyohitimu darasa la VII ……………….....………................... Wilaya……....…................... Mkoa….....………....
Mwaka wa kuhitimu Elimu ya msingi ................................. Daraja lako la ushindi darasa la saba: ............................
Sekondari ya serikali uliyopangiwa ............................................ Wilaya ....................................... Mkoa .....................

Dini yako: *Mwislamu*/*Mkristo* (kata mojawapo)
Madhehebu: *Kilutheri*/*Roman*/*Anglican*/*Moravian*/*Shiha*/ au ……………………………….................

### 2.0 FAMILIA YA MWANAFUNZI (*Ijazwe na Mzazi/Mlezi*)

### 2.1. Mzazi /Mlezi

Jina la Baba/Mlezi …………….................................…........................ Simu: ..........................................................
Jina la Mama/Mlezi ……………………………………………...............Simu…...................……………………........
Kazi ya Baba/Mlezi...................................................................Kazi ya Mama/Mlezi……………..........................……
Anwani ya Posta: ……...........……………………………….........................................................................................
Dini au Madhehebu ya wazazi: Baba ………………………….............. Mama: ..........................................................
Kabila la Baba (linahitajika katika kitabu cha usajili wa wanafunzi): ..........................................................................

### 2.2 Ndugu au marafiki wa familia

Tafadhali jaza majina ya ndugu /marafiki wa familia wasiozidi 4 wanaoruhusiwa kumtembelea au kushirikishwa raha, shida au hitaji la mtoto akiwa shuleni. Mzazi ukiwa mbali ila una jamaa wa karibu na shule ni vyema kumuandika huyo**. Hapa usiandike jina la baba au mama au mlezi maana hao tayari wameandikwa juu.**

| JINA | UHUSIANO | ANAKOISHI | NAMBA SIMU |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

### 3. TAARIFA YA PEKEE YA MZAZI NA AHADI

Je, mzazi, mwanetu ana tabia mbaya yoyote unayopenda tumsaidie? Kama anayo eleza na ikibidi ushauri asaidiweje.
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………

**4. KUKUBALI MAELEKEZO NA KUJIUNGA NA SHULE**

(*Ijazwe na mwanafunzi na mzazi baada ya kusoma na kuelewa vema maagizo ya kujiunga*)
Baada ya kusoma na kuelewa maagizo ya kujiunga na BUKOBA HOPE LUTHERAN
Mimi …………………….......................................................................................................................
ninaahidi kuwa nitafuata sheria za shule na maagizo mengine yatakayotolewa na uongozi wa shule.

…………………………............... ……………………..
**Saini ya Mwanafunzi** **Tarehe**

Baada ya kusoma na kuelewa maagizo ya mwanangu kujiunga na Bukoba Hope Lutheran, ninamruhusu kujiunga na shule hii. Ninaahidi kumtimizia mwanangu mahitaji ya shule ili ajiunge na kuendelea na masomo shuleni hapa Bukoba Hope Lutheran.

……………………………… ………………………. …………….
**Jina la Mzazi/Mlezi** **Saini ya Mzazi/Mlezi** **Tarehe**

**********************************************************************************************
**********************************************************************************************

**5. AFYA YA MWANAFUNZI**

Mimi Dr/Tabibu ………………………………………………………………….. wa Hospitali ya au Kituo cha Afya cha …………………………………………………………………………………………….
nimempima afya (Jina la mwanafunzi) ……………………………………………………………….. na nimebaini **ana/hana** ugonjwa (taja ugonjwa kama anao) ………………………………………………….
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………...
Ushauri wa Daktari/Tabibu: ……………………………………………………………………….........
……………………………………………………………………………………………………….………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………….

**SAHIHI YA DAKTARI/TABIBU**
**NA MHURI**

*Ikiwa mtoto amekwishapimwa afya kwa kutumia fomu ya shule nyingine, asipimwe tena ila badala yake alete fomu ya shule nyingine yenye taarifa ya afya yake.

Rev. J. Mwesigwa Kyaruzi
**MKUU WA SHULE 0754 264 200 / 0759742310**